
# Maagizo ya Kikaragosi

Kila siku ya shule ya Biblia ya likizo ya shambani kuna onyesho la kikaragosi la farasi na jogoo.Vikaragosi hawa wawili watahudhuria tukio lako na kushiriki. Onyesho la kikaragosi hufanyika mwishoni mwa programu, na hutumika kuchunguza somo walilojifunza wanafunzi.Tunafurahia kukupa maelekezo yote yanayotakiwa ili kuunda vikaragosi hawa 2: farasi na jogoo.Wataleta msisimko wa aina yake na kusaidia wanafunzi wako kuchunguza somo na kurudi nyumbani wakiwa tayari kuwasimulia wazazi wao kile walichojifunza.

1. Kusanya vifaa unavyohitaji.
   - Mkasi
   - Penseli (ya kuchora kiolezo kwenye kitambaa)
   - Gundi (inayofanya kazi kwa haraka, inafanya kazi katika kitambaa: Gundi ya silikoni au ya moto)
   - Vijazo
   - Kadibodi (si lazima)
   - Uzi na sindano
   - Waya: mita 1½





2. Pakua karatasi tano za kiolezo za PDF na uchapishe kwa kutumia karatasi ya 11x17 au A5 kwa zile kubwa, na karatasi ya 8.5 x 11 au A4 kwa zile ndogo.
   - Kiolezo cha kichwa cha farasi
   - Kiolezo cha ziada cha farasi
   - Kiolezo cha Kichwa cha Jogoo
   - Kiolezo cha ziada cha jogoo
   - Kiolezo cha ubawa wa jogoo

3. Nunua kitambaa kinachohitajika kwa farasi na jogoo. Tunapendekeza kitambaa gandamizo, kwa sababu ni imara na hakichakai. Hata hivyo, unaweza kutumia kitambaa chochote unachoweza kupata kwa urahisi katika eneo lako. Tunapendekeza kitambaa imara.
   Kiasi cha kitambaa hapa chini ni makadirio tu, enda kwa duka pamoja na violezo unaponunua kitambaa ili kuhakikisha umepata kiasi cha kutosha.
   - Cha kahawia: mita 1/2
   - Chekundu: mita 1/8
   - Cha rangi ya machungwa: mita 1/2
   - Cheupe: mita 1

# Maagizo ya Kikaragosi cha Farasi:


1. Kata kitambaa ili kutengeneza mwili na kinywa cha farasi.
   - Kata vipande viwili vya mwili wa farasi katika kitambaa cha kahawia.
     * Kumbuka kuongeza sentimita 3 chini ya kiolezo.
   - Kata kinywa 1 katika kitambaa chekundu.





2. Shona pamoja vipande vikuu
   - Shona pamoja miili miwili ya farasi kwa kutumia uzi wa kahawia (lakini usishone kinywa pamoja, au chini ya shingo ambapo mkono wako utaingia).
   - Shona kinywa chekundu kwenye kinywa cha farasi wa kahawia. (Tazamaa video kwa maelekezo zaidi.) Tumia vipeo vya pembetatu ili kuoanisha kingo kwa usahihi.






3. Geuza farasi aliyeshonwa, ili mishono iwe upande wa ndani.

4. Chagua mitindo ya masikio, manyoya na pua .Kata vipande kwa kutumia kiolezo au tumia mtindo wako.



5. Gandisha masikio, manyoya na pua. Tulitumia gundi ya moto (silikoni), kwani ilikuwa rahisi kuliko kushona kwa kuunganisha vipande.

6. Gandisha nywele ya rangi ya machungwa, kisha kata ili kutengeneza vipande vidogo vya nywele. Gandisha macho ya kusonga au tumia vijiko vya plastiki kama inavyoonyeshwa kwenye picha. Tulitumia vijiko vyeupe vya kutupa kama jicho (tulitoa mpini) na kupaka rangi nyeusi katikati kama mboni ya jicho.

7. Kata sikio kutoka kitambaa cha kahawia, kisha kata sikio ndogo kutoka kitambaa cha rangi ya machungwa kama inafaa. Shikanisha sikio pamoja sehemu ya chini, kisha gandisha kwenye kichwa.

8. Kata vipande vya pua na kugandisha upande wa mbele wa kikaragosi


9. Tumia vijazo vya mto ili kujaza kichwa.Weka upande wa mbele wa pua katika sehemu ya ndani ambapo utaingiza mkono wako.Unaweza pia kugandisha kadibodi upande wa ndani ili kufanya kinywa kuwa imara ikiwa inafaa.

Umepata kikaragosi cha farasi!

## Maelekezo ya Kikaragosi cha Jogoo:

1. Kata kitambaa kwa ajili ya mwili na mdomo wa jogoo.
    - Kata vipande viwili vya mwili wa jogoo kutoka kitambaa cheupe.
      * Kumbuka kuongeza sentimita 10 chini ya kiolezo.*
    - Kata mdomo 1 katika kitambaa cha kahawia.







2. Shona pamoja miili kwa kutumia uzi mweupe.

3. Shona vipande viwili vya rangi ya machungwa vya mdomo kwenye sehemu ya mdomo wa mwili mweupe.



4. Shona mdomo wa kahawia ndani ya mdomo wa rangi ya machungwa. Baada ya kumaliza kushona, geuza ili upande wa ndani kuwa nje.






5. Chagua mitindo ya kishungi, shavu na macho.Kata vipande kwa kutumia kiolezo na kutengeneza mtindo wako.




6. Gandisha kishungi, shavu na macho .Tulitumia gundi ya moto, kwani ni rahisi zaidi kuliko kushona kwa kuunganisha vipande.




7. Weka vijazo kwenye kichwa ikiwa unataka.

8. Shona au gandisha mabawa katika pande za kikaragosi chako.

9. Tumia mraba mdogo wa kitambaa cheupe ili kugandisha juu ya waya. Tumia gundi ya silikoni au ya moto kwa kushika waya kati ya kitambaa, na itaonekana vizuri.



Umepata kikaragosi cha jogoo!